

**HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA RUKWA
MHESHIMIWA ZELOTE STEPHEN ZELOTE
KWENYE MAADHIMISHO YA SIKU YA
UPANDAJI MITI KATIKA HALMASHAURI YA
WILAYA YA SUMBAWANGA
TAREHE 19 JANUARI, 2016**

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Chama cha
Mapinduzi Mkoa,

Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya,

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya
ya Sumbawanga,

Watumishi wote wa Serikali,

Ndugu Wananchi,

Mabibi na Mabwana.

Kwanza kabisa nitumie fursa hii kuwashukuru
kwa kunialika kuwa mgeni rasmi kwenye
maadhimisho haya muhimu. Pili, niwapongeze

ninyi nyote mliotenga muda wenu kwa ajili ya kufika kwenye maadhimisho haya. **Asanteni sana.**

Ndugu wananchi,

Mkoa wa Rukwa una maeneo ya misitu ya asili iliyohifadhiwa kisheria yenye ukubwa wa hekta 134747.9 na misitu ya kupandwa ukubwa wa hekta 5205.5. Katika msimu huu wa mvua tunatarajia kupanda jumla ya miti 2,343,500 ya aina mbalimbali katika mkoa. Hadi kufikia tarehe 15 Januari, 2017 jumla ya miti 2,082,602 ilikuwa imepandwa. Hii ni sawa na asilimia 88.9 ya lengo.

Ndugu wananchi,

Bila shaka mnatambua kuwa Miti ni rasilimali muhimu sana katika maisha ya mwanadamu. Miti husaidia katika upatikanaji wa mvua, hupunguza hewa ya ukaa kwenye mazingira yetu, hutunza

ardhi, hutupatia hewa safi ya oksijeni lakini pia mazao ya miti kama mbao, mkaa na kuni; hizi ni baadhi tu ya faida za miti.

Pamoja na faida hizo jamii zetu zimekuwa zikua zikitoa umuhimu mdogo wa kupanda na kutunza miti katika Mkoa ndio maana ikawekwa siku ya upandaji miti kitaifa na Mkoa ili kutukumbusha suala hili muhimu la kutunza na kuwekeza kwenye rasilimali za miti.

Ndugu Wananchi,

Mkoa wa Rukwa umejaliwa kuwa na eneo kubwa la ardhi ambalo linafaa kwa upandaji miti lakini pamoja na kuwa na fursa hiyo bado hatujaichangamkia kwani kasi yetu ya kupanda miti ni ndogo sana. Vilevile kumekuwa na matukio ya uchomaji miti ovyo, ukataji miti kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kijamii bila kufuata

sheria. Zote hizo ni changamoto ambazo zinaathiri misitu na tahadhari zisipochukuliwa athari zake zitapelekea Mkoa wetu kukumbwa na tatizo la ukame hapo baadaye na kugeuka jangwa.

Ndugu Wananchi,

Mikoa ambayo tunaona inakumbwa na ukame katika kipindi hiki; hali ilianza kwa kukata miti na kutopanda hivyo kupelekea uharibifu wa mazingira ambao umepelekea mikoa hiyo kuwa kame. Sisi kama Serikali ya Mkoa wa Rukwa hatutaruhusu hali hiyo kutokea katika Mkoa wetu, hivyo ni muhimu kila mwananchi kutekeleza Sheria.

Ndugu Wananchi,

Mkoa unatekeleza mkakati wa kukabiliana na changamoto nilizozitaja hapo juu. Mkakati huo unajumuisha mambo yafuatayo:-

1. Taasisi zote zilizopo kwenye maeneo yetu kama Shule, Zahanati, Makanisa, Misikiti kupanda miti kwenye maeneo yao,
2. Kila Halmashauri, Kata na Kijiji kuandaa vitalu vya miti ambavyo vitazalisha miche ya kupanda maeneo mbalimbali,
3. Kila mtu ahakikishe anapanda miti kwenye eneo lake kila ifikapo msimu wa mvua,
4. Wananchi wote waliovamia kwenye maeneo ya hifadhi ya misitu kuondolewa mara moja,
5. Wananchi kutekeleza Sheria za usimamizi wa rasilimali za misitu katika maeneo yao na kutoa ushirikiano kwa Serikali ili kuwafichua wale wote wanaovunja Sheria hizo,
6. Wakala wa misitu (TFS) Mkoa wa Rukwa kuendelea kusimamia Sheria, kuzalisha miche ya miti kwa ajili ya kupanda na kupanda miti kwenye maeneo mbalimbali waliyotengewa.

Ndugu Wananchi,

Tukitekeleza mambo hayo tutakuwa tumetatua au kupunguza changamoto zinazotukabili kwa upande wa misitu na itatusaidia kutunza mazingira yetu. Hivyo ni muhimu kwenu ninyi wananchi kushirikiana na Serikali katika kutekeleza mkakati huu.

Mwisho kabisa nawatakia utekelezaji mwema wa upandaji miti ili kufanya Mkoa wetu kuwa Mkoa wa kijani. Kila mtu ashiriki katika kupanda miti kwenye eneo lake kwa kadri ya uwezo wake, nina imani tutafanikiwa.

Ahsanteni kwa kunisikiliza.